SHERIA
YA
KUFUTA SHERIA YA TUME YA UCHAGUZI
NAM. 9 YA 1992 NA KUTUNGA SHERIA YA KUANZISHA
AFISI YA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR, MAJUKUMU,
UWEZO NA MAMBO MENGINE
YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA UTANGULIZI**

1. Jina fupi na kuanza Kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**TUME YA UCHAGUZI**

3. Kuanzishwa na Muundo wa Tume.
4. Kazi za Tume.
5. Uwezo wa Tume kusimamia kampeni za uchaguzi.
6. Uwezo wa kutaka taarifa.
7. Uwezo wa Tume kutumia jengo au eneo.
8. Uwezo wa kuanzisha kamati za ushauri.
9. Uwezo wa kuruhusu waangalizi.
10. Uwezo wa kutunga kanuni na miongozo.

**SEHEMU YA TATU**
**UANZISHAJI WA AFISI NA KAZI ZAKE**

11. Kuanzishwa kwa Afisi.
12. Muhuri na nembo ya Afisi.
13. Mkurugenzi.
14. Sifa za Mkurugenzi.
15. Muda wa Utumishi wa Mkurugenzi.
16. Kazi za Mkurugenzi.
17. Kurugenzi.
18. Sekretarieti.
19. Kuanzishwa Afisi za Uchaguzi za Wilaya.
20. Kazi za Afisa Uchaguzi wa Wilaya.
21. Watumishi wengine.
22. Uhamisho wa wafanyakazi.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA


23. Bajeti.
24. Fedha za Tume.
25. Afisa Muhasibu.
26. Hesabu na Ukaguzi.


## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO


27. Ripoti.
28. Fidia ya ajali.
29. Makosa na adhabu.
30. Kutoa taarifa za Afisi.
31. Kinga kwa maafisa wa Tume.
32. Malipo ya Wajumbe na Maafisa wa Tume.
33. Kanuni.
34. Kufuta na Kubakiza.

**SHERIA NAMBA 1 YA 2017**

**NIMESAINI**

Alhemi

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

28 Machi, 2017

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TUME YA UCHAGUZI NAM. 9 YA 1992 NA KUTUNGA SHERIA YA KUANZISHA AFISI YA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR, MAJUKUMU, UWEZO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.**

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2017, na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo-

"Mgombea" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Tume kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar au Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani;

"Tume" maana yake ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 119(1) cha Katiba;

"Katiba"maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 119(1)(a) cha Katiba;

"Jimbo" maana yake ni kuhusiana na uchaguzi wowote isipokuwa wa Rais, ni jimbo kwa madhumuni ya uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi au Serikali za Mitaa na kwa uchaguzi wa Rais ni Zanzibar yote;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Uchaguzi aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha Sheria hii;

"Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya" maana yake ni Afisa aliyeteuliwa kufanya kazi za Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria hii na inajumuisha Afisa Msaidizi wa Uchaguzi;

"Uchaguzi" maana yake ni kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Uchaguzi;

"Mjumbe" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 119(1) cha Katiba;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Uchaguzi;

"Mkuu wa Kurugenzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Tume kusimamia majukumu ya idara ikijumuisha Msaidizi wake;

"Kurugenzi"maana yake ni kurugenzi za Tume kama inavyoainishwa katika kifungu cha 17 (1) cha Sheria hii;

"Afisi" maana yake ni Afisi ya Tume iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria hii;

"Chama" maana yake ni Chama cha Siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Siasa ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania;

"Rais"maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Kura ya maoni" maana yake ni utaratibu wa kupeleka suala au hoja kwa wapiga kura ili watoe uamuzi;

"Sekretarieti" maana yake ni Sekretarieti ya Tume iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria hii;

## SEHEMU YA PILI
## TUME YA UCHAGUZI

Kuanzishwa na Muundo wa Tume

**3.** Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo muundo na majukumu yake itakuwa kama ilivyoainishwa katika Katiba.

Kazi za Tume

**4.**-(1) Tume itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa uchaguzi na kura ya maoni ndani ya Zanzibar.

(b) kusimamia, kukuza na kuratibu elimu ya wapiga kura;

(c) kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(d) kufanya mapitio na kuweka mipaka ya majimbo; na

(e) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyopewa chini ya masharti ya Sheria hii au Sheria nyengine au Kanuni.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao, Tume itaandaa, kuweka na kupendekeza muundo wa Tume ya Utumishi na watendaji wake utakaozingatia sifa na majukumu ya kila mtendaji.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume itatekeleza kazi zake kwa kufuata Katiba, Sheria na Misingi ya Demokrasia na Utawala Bora.

Uwezo wa Tume kusimamia kampeni za uchaguzi.

**5**. Katika kutekeleza kazi zake, Tume itakuwa na uwezo wa kusimamia kampeni za uchaguzi.

Uwezo wa kutaka taarifa.

**6.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote inayohusiana na masuala ya Usalama wa Taifa, Tume inaweza kwa maandishi kuomba, kutoka kwa mtu au taasisi yoyote taarifa yoyote ambayo inaamini mtu au Taasisi hiyo inazo.

(2) Mtu yeyote, bila ya sababu ya msingi akishindwa kutoa taarifa kwa Tume kama ilivyoelekezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, au ametoa taarifa yoyote ambayo anajua kuwa ni ya uongo au amechelewesha kutoa taarifa hizo ndani ya muda, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi laki tano na isiyozidi Shilingi Milioni mbili, au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au faini na kifungo kwa pamoja.

Uwezo wa Tume kutumia jengo au eneo

**7.**-(1) Wakati wa kipindi cha uchaguzi au kura ya maoni, Tume baada ya kushauriana na wamiliki wa jengo au eneo, itakuwa na uwezo wa kutumia jengo au eneo kwa kazi za uchaguzi au kura ya maoni.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume haitatumia jengo au eneo lolote la ibada au eneo la chama kwa kazi za uchaguzi au kura ya maoni.

Uwezo wa kuanzisha kamati za ushauri

**8.**-(1) Tume inaweza, kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa majukumu yake chini ya Sheria hii, kuanzisha Kamati za ushauri kama itakavyoona inafaa.

(2) Katika kuanzisha kamati za ushauri, Tume itateuwa wajumbe kwa idadi na utaratibu maalumu kama itakavyoona inafaa.

(3) Kwa mujibu wa miongozo ya jumla au mahsusi, Tume itaratibu taratibu za mikutano ya kamati kama itakavyoainishwa kwenye Kanuni iliyotungwa chini ya Sheria hii.

Uwezo wa kuruhusu waangalizi

**9.**-(1) Tume inaweza, katika uchaguzi wowote au kura ya maoni, kwa maombi maalum, na baada ya kuridhika na sifa za muombaji, kutoa kibali cha uangalizi wa uchaguzi au kura ya maoni.

(2) Tume itatoa miongozo na masharti kwa taasisi iliyopewa kibali cha uangalizi, itakayoainisha madhumuni na masharti ya kibali na hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa taasisi itakayokiuka madhumuni na masharti ya kibali hicho.

(3) Taasisi yoyote itakayopewa kibali cha uangalizi chini ya kifungu hiki, itatakiwa kuwasilisha kwa Tume ripoti ya uangalizi inayoelezea namna uchaguzi au kura ya maoni ilivyoendeshwa na mapendekezo yake ndani ya siku tisini (90) baada ya kutangazwa matokeo.

(4) Taasisi yoyote ya uangalizi itakayoshindwa kuwasilisha ripoti ya uangalizi katika kipindi kilichoelezwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, haitopatiwa kibali cha uangalizi katika uchaguzi au kura ya maoni zinazofuatia.

(5) Mtu yeyote au taasisi yoyote itakayofanya uangalizi wa uchaguzi bila ya kibali cha Tume itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia itawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi milioni tatu na isiyozidi milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja au vyote faini na kifungo na hataruhusiwa kuomba tena kuwa mwangalizi wa Uchaguzi wa Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10.

Uwezo wa kutunga kanuni na miongozo

**10.** Tume inaweza wakati wowote mazingira yatakapohitaji, katika utekelezaji wa majukumu yake, kuandaa Miongozo.

## SEHEMU YA TATU
## UANZISHAJI WA AFISI NA KAZI ZAKE

Kuanzishwa kwa Afisi.

**11.**-(1) Kutakuwa na Afisi itakayojulikana kuwa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(2) Afisi itakuwa taasisi inayojitegemea, endelevu yenye muhuri na jina lake na itakuwa na uwezo wa:-

(a) kumiliki au kuhaulisha mali inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia katika mikataba au kufunga miamala yoyote; na

(c) kufanya au kuelekeza kufanywa jambo jengine lolote ambalo taasisi yenye kujitegemea inafanya au inaelekeza kufanywa.

Muhuri na nembo ya Afisi

**12.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Afisi kwa muundo na namna ambayo itaamuliwa na Tume.

(2) Matumizi ya muhuri wa Tume katika kila nyaraka yatatambulika ni sahihi ikiwa yametiwa saini na Mkurugenzi au Afisa yeyote wa Tume aliyeidhinishwa na Mkurugenzi.

(3) Nyaraka yoyote ambayo imetolewa na Tume ambayo imetiwa muhuri wa Tume kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itachukuliwa kwamba ni sahihi na ni nyaraka ya Tume ambayo itakubalika kuwa ni ushahidi ambao hauhitaji ushahidi mwengine kuuthibitisha.

Mkurugenzi

**13.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi, atakula kiapo cha utii na kutunza siri mbele ya Rais kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake.

(3) Mkurugenzi atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Afisi na Katibu wa Tume ambaye atatekeleza majukumu ya kila siku ya Afisi.

Sifa za Mkurugenzi

**14.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi iwapo :-

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu kinachotambulika; na

(c) ni Afisa Muandamizi katika Utumishi wa Umma.

Muda wa Utumishi wa Mkurugenzi.

**15.** Mkurugenzi atashika wadhifa wa ukurugenzi kwa mujibu wa masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma.

Kazi za Mkurugenzi

**16.**-(1) Bila ya kuathiri kazi za Tume zilizoainishwa kwenye kifungu cha 4 cha Sheria hii, Mkurugenzi atatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) kusimamia na kutekeleza kazi za kila siku za Afisi;

(b) kuandaa na kuratibu Mikutano ya Tume;

(c) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Tume katika kutekeleza majukumu yake;

(d) kuandaa bajeti na kalenda ya shughuli za Tume;

(e) kuweka kumbukumbu za mikutano ya Tume;

(f) kutayarisha nyaraka za kazi za Tume;

(g) kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi ambazo zinafanya kazi za uchaguzi, demokrasia na utawala bora;

(h) kutoa na kusimamia miongozo kwa maafisa wa uchaguzi katika kutekeleza majukumu yao kama itakavyoagizwa na Tume;

(i) kusimamia nidhamu za watendaji wa Afisi;

(j) kufanya tafiti zinazohusiana na uchaguzi au kura ya maoni; na

(k) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoagizwa na Tume kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Katika kutekeleza kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi atasaidiwa na watendaji wengine wa Sekretarieti.

Kurugenzi

**17.**-(1) Tume, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, itaanzisha kurugenzi za Afisi kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake.

(2) Kila kurugenzi itakuwa na Mkuu atakaeteuliwa na Tume miongoni mwa watendaji waandamizi watakaopendekezwa na Mkurugenzi.

(3) Mkuu wa kurugenzi atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa maelekezo ya Mkurugenzi.

Sekretarieti

**18.**-(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Tume ambayo itakuwa na jukumu la kuisaidia Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Sekretarieti itaundwa na wajumbe wafuatao-

(a) Mkurugenzi ambaye atakuwa ni kiongozi wa Sekretarieti;

(b) Wakuu wa Kurugenzi; na

(c) Maafisa wengine kama itakavyoelekezwa na Tume.

(3) Sekretarieti inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria vikao vyake kwa madhumuni ya kutoa maoni yake ya kitaalamu.

Kuanzishwa Afisi za Uchaguzi za Wilaya.

**19.**-(1) Kutakuwa na Afisi ya Uchaguzi ya Wilaya kwa kila Wilaya ya Zanzibar, itayosimamiwa na Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya.

(2) Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya ataajiriwa na Tume kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa msimamizi wa jimbo au majimbo katika Wilaya yake katika kipindi cha Uchaguzi.

(4) Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya kabla hajaanza kazi zake atalazimika kula kiapo cha utendaji kazi mbele ya Hakimu.

Kazi za Afisa Uchaguzi wa Wilaya.

**20.** Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) kuandikisha wapiga kura;

(b) kuhamisha taarifa za mpiga kura kutoka sehemu moja na kuzipeleka sehemu nyengine;

(c) kurekebisha makosa ya taarifa za mpiga kura kwenye daftari la wapiga kura;

(d) kuandaa kampeni za uelewa wa masuala ya uchaguzi na elimu kwa mpiga kura;

(e) kuratibu shughuli za elimu kwa mpiga kura katika Wilaya yake;

(f) kusimamia shughuli za uchaguzi na kura za maoni; na

(g) kutekeleza jambo lolote kama litakavyoamuliwa na Tume kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote.

Watumishi wengine

**21.** Tume inaweza kuajiri watumishi wengine wa Afisi kwa kadri itakavyoona inafaa kulingana na mahitaji na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Uhamisho wa wafanyakazi.

**22.** Kwa ajili ya kuhakikisha uhuru wa Tume na uwazi wa Afisi, Afisa isipokuwa yule aliyeteuliwa na Rais, hatohamishwa bila ya ridhaa ya Tume.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Bajeti

**23.** Afisi itakuwa na bajeti yake maalumu kwa fedha ambazo zitaidhinishwa au kutengwa kwa ajili ya matumizi ya Afisi.

Fedha za Tume

**24.**-(1) Kutakuwa na fedha za Tume ambazo zitajumuisha:-

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi; na

(b) fedha zitakazopewa Tume kwa njia ya msaada, michango au aina nyengine yoyote ya fedha halali.

(2) Mkurugenzi anaweza, baada ya kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya fedha, kuandaa utaratibu wa kuchangia fedha kwa ajili ya shughuli za uchaguzi.

Afisa Muhasibu

**25.** Mkurugenzi atakuwa Afisa Muhasibu wa Afisi.

Hesabu na Ukaguzi

**26.**-(1) Mkurugenzi atatunza vitabu vya hesabu na stakabadhi zote na matumizi yote ya Afisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya fedha za Umma.

(2) Akaunti za Afisi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Mkaguzi yeyote aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na taarifa za ukaguzi huo pamoja na taarifa za fedha zitawasilishwa kwa Waziri.

## SEHEMU YA TANO

## MASHARTI MENGINEYO

Ripoti

**27.**-(1) Tume, mara baada ya uchaguzi mkuu au kura ya maoni, itatayarisha ripoti inayohusiana na uchaguzi au kura ya maoni na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili (12).

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ripoti itakuwa na mambo yote muhimu ya Uchaguzi Mkuu au kura ya maoni kwa kadri inavyowezekana, na taarifa nyengine zozote ambazo Tume inaona inafaa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Tume kila baada ya miaka mitano itatayarisha ripoti ya utekelezaji wa kazi zake na kuiwasilisha kwa Rais.

Fidia ya ajali

**28.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, mjumbe wa Tume au mtendaji mwengine atakaepata ajali au kujeruhiwa wakati akitekeleza kazi za Uchaguzi au kura ya maoni atakuwa na haki ya kupata fidia kutokana na ajali hiyo kama itakavyoelezwa na Kanuni.

Makosa na adhabu

**29.** Mtu yeyote ambaye-

(a) kwa makusudi atamzuia mjumbe wa Tume au Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Tume kutekeleza majukumu yake; au

(b) kwa makusudi ataharibu mwenendo wa mkutano wa Tume au kufanya vitendo vitavyopelekea mkutano wa Tume usiendelee; au,

(c) atafanya jambo jengine lolote litalosababisha Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii;

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano na isiyozidi Shilingi Millioni Moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kutoa taarifa za Afisi

**30.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi atatoa taarifa yoyote ya Afisi kwa mtu yeyote asiyehusika, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi laki tano na isiyozidi Shilingi Millioni Tano au atatumikia kifungo cha miaka mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kinga kwa maafisa wa Tume

**31.** Kitendo chochote kilichofanywa au kimeachwa kufanywa kwa nia njema na Afisa wa Tume katika utekelezaji wa kazi au uwezo wake chini ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote, Afisa huyo hatokuwa na hatia ya madai au jinai kuhusiana na tendo hilo.

Malipo ya Wajumbe na Maafisa wa Tume.

**32.**–(1) Malipo ya Wajumbe wa Tume yatalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kiwango ambacho kitaamuliwa na Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Afisa wa Tume atalipwa mshahara kama itakavyoamuliwa na Tume kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kanuni

**33.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

(2) Kanuni yoyote itakayotungwa chini ya Sheria hii itatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali

Kufuta na Kubakiza

**34.**-(1) Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Namba 9 ya 1992 inafutwa.

(2) Bila ya kujali Sheria iliyofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa, au tendo lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 16 Februari 2017.

.............................................
RAYA ISSA MSELLEM
***Katibu, Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar***